

## Kuwasiliana na Huduma ya Polisi ya Edmonton

Piga 9-1-1 kwa huduma za dharura pekee.

Kwa huduma zisizo za dharura piga 780-423-4567

Kupatikana kwa rununu: #377

Kiziwi au ugumu wa kusikia: 780-425-1231

Kwa habari zaidi, tembelea: [edmontonpolice.ca](http://edmontonpolice.ca)

Ungana kwenye  
mitandao ya kijamii



EDMONTON  
**POLICE**  
SERVICE

[edmontonpolice.ca/KnowYourRights](http://edmontonpolice.ca/KnowYourRights)

## Unaposimamishwa na afisa wa polisi:

- Hauhitajiki kujibu maswali ya afisa wa police
- Unahitajika kujitambulisha iwapo una vunja sheria - Hii inajumisha sheria za serikali za manispali na sheria za mikoa ambazo zinahitaji kutozwa kwa tikiti- au iwapo unakamatwa
- Unaweza kusema 'hapana' afisa wa polisi anapouliza kama anaweza pekua mizigo yako iwapo haujakamatwa ama kuzuiliwa kwa sababu za usalama
- Unaweza kuondoka iwapo haujazuiliwa au kukamatwa
- Iwapo umekamatwa au umezuiliwa, ni haki yako kuongea na wakili wako punde tu afisa wa polisi anatakupa na usalama wa kufanya hizi kulingana na hali yako
- Una haki ya kujua jina la afisa wa polisi au nambari yake ya usajili iliyoko kwenya beji
- Hauhitajiki kuwa ruhusu polisi kuingia kwako nyumbani iwapo hawana nakala ya hati ya utaftaji au jambo la dharura

*Ujumbe huu unalenga kutoa maagizo jumla kuhusu mwingiliano wa raia na afisa wa polisi. Huu si ujumbe kamili wa haki za raia. Ujumbe huu hauondoi ushauri wa wakili ambaye anaweza kupa mashauri kamili kulingana na hali yako. Unafaa uzungumze na wakili akupe mawaidha kuhusiana na hali yako. Iwapo utakamatwa, afisa wa polisi anatakusomea haki zako na atakupa nambari isiyotozwa ada ili uweze kupata huduma ya abure ya wakili pamoja na chochote kile ambacho utapata kikiwa cha msaada.*

- Unaweza kuitisha nakala ya hati ya utaftaji inayo ruhusu afisa wa polisi kuingia nyumbani kwako
- Unahitajika kutoa leseni yako udereva, usaliji wa gari na bima utakapo simamishwa unapoendesha gari
- Hauna haki ya kuongea na wakili wako kabla ya kupima kiwango cha ulevi kupitia pumzi barabarani
- Unaweza kumshtaki afisa wa polisi kwa afisa mkuu au kwa tume ya Polisi ya Edmonton iwapo umedhulumwa, umetendewa mambo yasiyo ya haki au iwapo haki zako zimekiukwa



## Wajibu wa Afisa wa EPS na Haki za Umma

Kuzuia kwa uhalifu ni muhimu katika kuzingatia wa usalama wa raia. Jukumu la huduma ya polisi ya Edmonton (EPS) ni kulinda maisha na mali, kuzingatia amani ya umma, na kuzia, kugudua ana tatua uhalifu. Ambapo huduma ya Polisi ya Edmonton haina uwezo wa kuzuia uhalifu ikishirikiana na jamii, lengo letu huwa ni kuuchunguza.

Kila mtu ana haki ya kujiskia salama. Msingi wa utendakazi wa polisi ni kuaminiwa na umma na iwapo hakuna uaminifu polisi hawawezi kufanya kazi yao kikamilifu. EPS inahitajika kuelewa matatizo ya eneo lake na ifanye kazi na jamii kuzuia uhalifu kufanyika, ikiwa na lengo la kuimarisha maisha ya kila mtu aliye Edmonton.

Mazungumzo kati ya mtu na afisa wa police ni muhimu kwa kuwa yanaipa EPS habari ambazo zinaweza kusaidia kutatua na kuzuia uhalifu. Iwapo kuna mwingiliano na afisa wa polisi, mtu ana uhuru wa kuondoka na kuendelea na shughuli zake. Hata hivyo, hii haimzuii afisa wa polisi kujaribu kuzungumza na mtu lakini mtu ana uhuru wa kuondoka iwapo afisa wa polisi hana sababu ya kumkamata.

Afisa wa Polisi kutoka EPS anahitajika kujihusisha na umma iwapo wana-taka kuelewa jamii ambayo wanaitumikia. Jambo hili kwa mara huhusisha kuanza mazungumzo na mtu yeyote.

Afisa wa EPS wameelimishwa kufuata sera ambazo zinazingatia utendakazi wa polisi ulio wa haki bila upendeleo. Kwa mfano, msako barabarani unaweza kufanyika iwapo utasaidia katika uchunguzi, kuzuia uhalifu, machafuko na uonevu.

Ni muhimu sana kujua haki zako, na pia kujua majukumu ya afisa wa EPS mnapoingiliana. Yafuatayo yametengenezwa kukupa wewe habari kuhusu kile ambacho Afisa anapaswa kufanya, kile ambacho si lazima ukifanye na kile ambacho unaweza kufanya wakati ambapo utajipata katika matukio yanayo husisha polisi.

## Unaposimamishwa na afisa wa EPS ama anapo kukaribia ili azungumze na wewe analazimika:

- Kujitambulisha
- Kukueleza sababu ya kukusimamisha au sababu ya kutaka kuongea na wewe
- Iwapo unakamatwa au umezuiliwa, waeleze sababu

- Akupe ushauri kwamba unaweza kuzungumza na wakili iwapo unakamatwa na kupe nafasi ya kufanya haya kwa faragha na usalama
- Kuwacha uendeleo na shughuli zako iwapo haujakamatwa au umezuiliwa.
- Akupe nakala ya hati ya utaftaji iwapo inayo wapa ruhusa wafanye upekuaji katika nyumba yako

- Wawe na busara na heshima wanapo fanya upekuaji
- Nguvu nyingi isititumike au waharibu mali bila sababu
- Warudishe mali yako katika miezi mitatu iwapo mali yako ilichukuliwa kama sehemu ya upekuaji na hauja hukumiwa kwa kukosa. Iwapo uchunguzi utazidi miezi mitatu, afisa wa polisi anahitaji ruhusa kutoka kwa hakimumu, ili andeleo kukaa na mali yako kwa ziadi ya miezi mitatu